

Notisi ya Kuongeza Eneo la Kutoa Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira (Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Tabora)

TANGAZOLA SERIKALI NA. 788 la tarehe 3/11/2023

SHERIA YA HUDUMA ZA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA,

(SURA YA 272)

NOTISI

(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 9(1) and (2))

NOTISI YA KUONGEZA ENEO LA KUTOA HUDUMA ZA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA (MAMLAKA YA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA TABORA), 2023

- | | |
|------------------------|---|
| Jina | 1. Notisi hii itajilikana kama Notisi ya Kuongeza Eneo la Kutoa Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira (Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Tabora), 2023. |
| Kuoneza eneo la huduma | 2. (1) Eneo la huduma la Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Tabora linaongezwa kujumuisha eneo lililoainishwa katika Jedwali la Notisi hii. |
| Kukoma kwa | 3. (1) Shirika la jamii au chombo kilicho sajiliwa Kwa ajili ya kutoa huduma za maji na usafi wa mazingira katika eneo la huduma linaloongezwa, baada ya kuanza kutumika kwa Notisi hii, litakoma kutoa huduma za maji na usafi wa mazingira katika eneo hilo.
(2) Bilakujaliaya ndogo ya (1) haki, majukumu, masharti ya ajira ya watumishi, mali, madeni na masuala mengine yanayofanana na hayo yaliyokuwa yakifanywa au yanayopaswa kufanywa na shirika la jamii au chombo kilichosajiliwa, yatabaki chini ya himaya ya Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira ya Tabora. |

JEDWALI

(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)

MAENEKO YA HUDUMA YANAYOONGEZWA

Mji wa Kaliua wenyewe jumla ya Kata tatu ambazo ni Kaliua, Ushokola na Ufukutwa.

Dodoma,
23 Oktoba, 2023

JUMAA H. AWESO
Waziri wa Maji

*Notisi ya Kuongeza Eneo la Kutoa Huduma za Maji na Usafi wa
Mazingira (Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Tabora)*
